

Homa ya Mafua,

Uchovu baada ya kunywa pombe  
nyingi

Au

Ugonjwa wa uti wa mgongo?

Mwangelie rafiki yako

Unaweza kuwa umepata chanjo ya MenC ambayo hukuinga dhidi ya ugonjwa wa uti wa mgongo wa aina ya C, lakini kuna vijidudu vingine ambavyo vinasababisha ugonjwa wa uti wa mgongo na ugonjwa wa kuoza damu kwa sababu ya vijidudu. vinasambazwa kupitia **kikohozi, kupiga chafya** na kugusana na watu kwa karibu kwa mfano kupitia **busu**. Muibuko hutokea mara nyingi katika sehemu ambazo watu wanaishi au kufanya kazi kwa karibu katika vikundi vikubwa.

Jambo muhimu la kujua ni kwamba magonjwa ya **uti wa mgongo na ya kuoza damu kwa sababu ya vijidudu yanaweza kuambukizwa na kuenea haraka sana**, wakati mwingine katika muda mfupi wa masaa.

Lakini, tatizo kuu, ni kwamba ishara za mwanzo sio kali na zinafanana na zile ambazo unapata kutokana na mafua au uchovu unaotokana na kunywa pombe nyingi, kwa mfano:

- **Kutapika;**
- **Kujihisi ukiwa na joto;**
- **Maumivu ya mgongo na viungo;**
- **Kuumwa na kichwa;**
- **Na shingo iliyokaza**

Lakini ukipata ishara zifuatazo:

- **Kutopenda mwanga kabisa**
- **Kuchanganyikiwa**
- **Vipelepele vidogo ambavyo haviishi ukizifinya; ama**
- **Koma.**

**Pata usaidizi wa matibabu haraka- matibabu ya mapema huokoa maisha**

**Ukiwa macho na kuwaangalia marafiki zako, na huogopi kuwauliza wanajihisi je, unaweza kuwa unaokoa maisha yao.**

Kijikaratasi hiki kinawezakupatikana kutoka [www.wales.gov.uk/immunisation](http://www.wales.gov.uk/immunisation) ama [www.cymru.gov.uk/imiwneiddio](http://www.cymru.gov.uk/imiwneiddio) katika lugha zifuatazo:

Kiarabu, Kibengali, Kibulgaria, Kichina, Czech, Kifarsi, Kifaransa, Kigujerati, Kihindi, Kikurdish (sorani), Kilingala, Kipoli, Kireno, Kipunjabi, Kirussia, Kisomali, Kispania, Kingereza, Kitgalog, Kiurdu, na Kivietnamu